## 4.0 KISWAHILI

Uchanganuzi wa matokeo ya mwaka wa 2014 umefanywa kwa kulinganishwa na yale ya miaka ifuatayo: 2011, 2012 na 2013.

***Jedwali 8: Matokeo ya KCPE Kiswahili ya 2011 hadi 2014***

| | **2011** | | **2012** | | **2013** | | **2014** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** |
| | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** |
| **Alama ya wastani** | 20.77 | 21.89 | 23.37 | 21.99 | 22.89 | 20.98 | 22.52 | 23.20 |
| **Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi** | 20 | 20 | 24 | 20 | 23 | 20 | 22 | 24 |
| **Alama ya juu iliyotuzwa** | 47 | 40 | 48 | 39 | 47 | 40 | 47 | 40 |

Jedwali hili linaonyesha kwamba:

**Katika lugha**:

a) Alama ya wastani yaelekea kubakia katika kiwango kilekile; **22.52** ikilinganishwa na **22.89** ya mwaka wa 2013.

b) Alama ya juu iliyoweza kutuzwa mwaka wa 2014 ni **47** sawa na **47** ya mwaka wa 2013.

c) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi ni **22** tofauti na **23** ya 2013.

d) Alama wastani haijafikia kiwango kinachokubalika (25/50).

**Katika Insha:**

a) Alama ya wastani ilipanda kutoka **20.98** mwaka wa 2013, hadi **23.20** mwaka 2014.

b) Alama ya juu zaidi iliyoweza kutuzwa mwaka wa 2014 ni **40** sawa na **40** ya mwaka wa 2013.


c) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi ni **24** tofauti na **20** ya mwaka wa 2013.

d) Alama wastani inaelekea kufikia kiwango kinachokubaliwa (**20/40**) japo imepita kiwango hiki kiasi.



*Powered by: www.manyamfranchise.com*


Mchoro ufuatao unaonyesha jinsi alama za sehemu za lugha na insha zilivyojitawanya.




## 4.1 SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

### 4.1.1 Uchanganuzi wa maswali maalum

Mchoro ufuatao unaonyesha asilimia ya watahiniwa ambao walipata jibu sahihi katika kila swali:




### 4.1.2 Uchanganuzi wa maswali yaliyowatatiza watahiniwa

Katika mwaka wa 2014, yapo maswali ambayo yalionekana kuwatatiza watahiniwa. Watahiniwa waliopata majibu sahihi kwa maswali haya walikuwa chini ya asilimia thelathini (30%). Maswali yafuatayo ndiyo yanayochukuliwa kuwa yaliwatatiza wanafunzi zaidi: Swali 4, 7, 16, 24, 27 na 34.



*Powered by: www.manyamfranchise.com*

*Jedwali 9: Maswali ambayo yaliwatatiza watahiniwa*

| Maswali | 4 | 7 | 16 | 24 | 27 | 34 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliopata jibu sahihi | 18.32 | 16.21 | 17.26 | 14.84 | 14.11 | 13.53 |
| Asilimia ya wastani ya mswali yale mengine | 22.36 | 20.79 | 24.28 | 24.04 | 24.33 | 21.38 |

### 4.1.3.1 Ruwaza za majibu

**Maswali 1 mpaka 15**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Usalama ni jambo __1__ kudumishwa kwa dhati; yaani __2__. Wizara husika __3__ kiasi maalum cha fedha kwenye bajeti ya taifa ili kugharamia shughuli za usalama. __4__ shughuli hizi ni kuwapa askari __5__ za kukabiliana na wakiuka sheria. __6__; uhifadhi wa usalama haupaswi kuachiwa polisi na wanajeshi pekee. Kila mwananchi sharti awajibike kupalilia amani; si kwa heri, si kwa shari, si kwa fanaka, si kwa __7__; wanajamii wote __8__ kukabiliana kila wakati na mtu yeyote anayezua vurugu.

**Swali la 4**

A. Baadhi ya B. Kati ya C. Mkabala na D. Pamoja na

**Matokeo ya swali la 4**

| Majibu | A | B* | C | D |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 63.37 | 18.32 | 3.12 | 8.80 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 23.17 | 22.36 | 19.81 | 19.10 |

Swali hili lilitahini vihusishi.Asilimia kubwa ya watahiniwa iliteua 'Baadhi ya' bila kuihusisha na matini jirani'. 'Baadhi ya' hutumiwa pale msemaji anapotarajia kutaja mambo mengi, wala si jambo moja. Ni muhimu walimu kufunza upya matumizi ya vihusishi ili wanafunzi waache kukanganyika.

**Swali la 7**

A. ukosefu B. shauku C. sikitiko D. uchungu

**Matokeo ya swali la 7**

| Majibu | A* | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 16.21 | 57.54 | 15.37 | 9.48 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 20.79 | 23.61 | 21.82 | 20.33 |

Swali hili lilitathmini uwezo wa mtahiniwa wa kuoanisha maneno katika msururu wa kauli na kuchanganua kinyume chake.Watahiniwa wengi walichagua jibu **B : shauku** ambalo si kinyume cha **fanaka.**Ni muhimu wanafunzi kusisitiziwa kusoma vifungu hivi kwa makini na kupima uwezekano wa jibu kabla ya kulitolea uamuzi.



*Powered by: www.manyamfranchise.com*

**Swali la 16**

Kukanusha kwa: 'Mtumbwi ambao ulinunuliwa umeanza safari,' ni:

A. Mtumbwi ambao ulinunuliwa haukuanza safari.
B. Mtumbwi ambao haukununuliwa haujaanza safari.
C. Mtumbwi ambao ulinunuliwa haujaanza safari.
D. Mtumbwi ambao haukununuliwa haukuanza safari.

**Matokeo ya swali la 16**

| **Majibu** | A | B | C* | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 3.83 | 58.68 | 17.26 | 18.92 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 19.30 | 22.99 | 24.28 | 20.27 |

Swali hili lilitahini ukanushaji.Yaelekea kwamba idadi kubwa ya wanafunzi ilikanusha vitenzi vyote viwili bila kubaini kwamba vitenzi hivi havitegemeani, hivyo havistahili kukanushwa vyote viwili.

**Swali la 24**

Chagua sentensi yenye maelezo sahihi.

A. Hijabu ni ugonjwa wa kuvimba fizi.
B. Kimeta ni ugonjwa unaodhoofisha figo.
C. Tauni ni ugonjwa unaokatakata viungo.
D. Surua ni ugonjwa wa kutoa vipele.

**Matokeo ya swali la 24**

| **Majibu** | A* | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 14.84 | 21.10 | 25.71 | 36.73 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 24.04 | 21.57 | 21.46 | 23.28 |

Swali hili lilitahini msamiati wa magonjwa.Asilimia kubwa ya wanafunzi ilichagua 'tauni' ambayo haisababishi kukatika kwa viungo.

**Swali la 27**

Chagua sentensi yenye maelezo sahihi.

A. Mjumu ni fundi wa kufua visu.
B. Sogora ni bingwa wa kuimba mashairi ngomani.
C. Dalali hushindania bidhaa mnadani.
D. Mkalimani hutafsiri maandishi vitabuni.



*Powered by: www.manyamfranchise.com*

**Matokeo ya swali la 27**

| Majibu | A* | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 14.11 | 24.32 | 30.72 | 29.34 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 24.33 | 20.79 | 23.31 | 22.36 |

Swali hili lilitahini msamiati wa wafanyakazi. Asilimia kubwa ya wanafunzi ilichagua 'dalali', ambaye huuza bidhaa mnadani wala hashindanii bidhaa zenyewe. Ni muhimu wanafunzi wahimizwe kusoma viteuliwa kwa makini.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **31** mpaka **40**.*

Afya au siha ni hali ya kutokuwa na maradhi. Hali hii humwezesha mtu kuhifadhi nguvu zake za mwili na kufanikisha utendakazi katika nyanja tofautitofauti. Mtu mwenye afya bora huweza kutekeleza mengi bila udhia. Mathalani, yeye huweza kujirausha na kujishughulisha hadi jioni bila kuhisi uchovu mwingi.

**Mti hauendi ila kwa nyenzo,** nayo afya nzuri haimjii tu mtu. Afya hustahili kupaliliwa na kutunzwa kwa namna anuwai kama vile kula vyakula vyenye viinilishe, kufanya mazoezi na kuandama mienendo miadilifu. Usafi wa mwili na mazingira pia huchangia katika kuimarisha afya. Ni wazi kwamba mazingira yakiwa machafu hukosa kuvutia na kusababisha kuhanikiza kwa harufu **inayokirihisha**. Isitoshe, uchafu huwa hali mufti ya kuzaana kwa wadudu kama vile chawa, kunguni, nzi na mbu ambao ni maadui wakuu wa afya.

Tabia ya mja huathiri afya yake. Wapo watu ambao wameambulia magonjwa kama vile saratani ya ini na mapafu, na kifua kikuu kutokana na uraibu wa pombe, sigara na dawa za kulevya. Wengine hujiponza kwa kuingilia vitendo viovu kama vile kushiriki mapenzi kiholela na kujisababishia magonjwa. Magonjwa haya ni kama vile kaswende na ukimwi ambao umewapukutisha wengi.

Hali kadhalika, watu hujiharibia afya kwa kufanya kazi mfululizo bila kupumzika. Licha ya kwamba bidii ni muhimu katika maendeleo ya jamii yoyote ile, utendaji kazi kidindia huweza kuwa na athari hasi. Kuna baadhi ya watu ambao wamewahi kupata maradhi ya moyo, ya kiakili na hata shinikizo la damu kutokana na hali kama hii. Wengine hujihasiri kwa kula vyakula vingi kupindukia. Kadhalika, wapo wengine ambao hupata magonjwa kwa kula vyakula visivyofaa. Katika kundi hili kuna wale ambao hawadiriki kufanya kazi wala mazoezi. Hawa hujinenepea na kudhoofisha utendakazi wao. Pia kuna wengine ambao hawali chakula cha kutosha. Hawa nao huweza kupata magonjwa kama vile safura na vidonda vya tumbo.

Hali ya umaskini pia huchochea kuzoroteka kwa afya. Asilimia kubwa ya watu nchini humu haimudu huduma bora za afya na lishe bora kutokana na hali ya ufukara. Wengine, kwa kukosa fedha, hawapati elimu ya kimsingi kuhusu afya. Hawa huweza kujizulia magonjwa kwa kutojua na kutofuata kanuni za afya. Pamoja na haya, kuna wale ambao wanarithi magonjwa ya kiukoo kama vile bolisukari kutoka kwa wazee wao.

**Umuhimu wa afya hauwezi kupuuzwa.** Taifa lenye kizazi chenye afya hustawi kiuchumi. Afya ikidumishwa wanajamii huweza kutumia fedha zao kuwekeza katika miradi badala ya kuzitumia kujiuguza au kuwauguza wenzao. Ni jukumu la kila raia kuhakikisha kwamba ameilinda afya yake na ya wengine kwa vyovyote vile. Walio na mazoea ya kupuuza ushauri wa wanaotoa huduma za afya na lishe wajiase, la sivyo watakuja kujiuma vidole.

**Swali la 34 .**

Chagua jibu ambalo **si sahihi** kulingana na aya ya **nne**.

A. Jambo jema huweza kusababisha hasara.

B. Kazi nyingi husababisha ugonjwa wa moyo.

C. Mazoezi hudhibiti ukubwa wa mwili.

D. Mapumziko huimarisha hali ya mtu kiakili..



*Powered by: www.manyamfranchise.com*

**Matokeo ya swali la 34**

| Majibu | A | B* | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 53.89 | 13.53 | 19.92 | 11.24 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 22.96 | 21.38 | 23.02 | 21.18 |

Hili ni swali la kiuchanganuzi .Mtahiniwa alihitajika kutumia ujuzi wa yaliyomo katika taarifa kuteua jibu sahihi.Watahiniwa wengi waliteua jibu **A,** pengine kwa kuwa hawajasoma kiini cha swali vyema, wakang'amua kuwa walihitajika kuteua jibu ambalo si sahihi. Linalojitokeza hapa ni kwamba wanafunzi wengi hawadiriki kusoma maswali kwa makini.

### 4.1.3.2 Hitimisho

Kwa jumla uchanganuzi wa mtihani wa mwaka 2014 umebainisha kwamba utendaji wa wanafunzi katika maswali ya ufahamu unaendelea kuimarika. Asilimia kubwa haikutatizika na maswali ya ufahamu kama ambavyo ilikuwa kawaida katika mitihani ya miaka ya awali. Hata hivyo, bado pana haja ya wanafunzi kufunzwa mikakati bora ya kukabiliana na maswali ya ufahamu.

Kadhalika, imebainika kwamba watahiniwa bado wanafanya vyema zaidi katika ufahamu wa kibunilizi ikilinganishwa na utendaji katika ufahamu wa kimaelezo.Ni muhimu walimu kuwaongoza wanafunzi zaidi katika kujibu maswali ya aina zote mbili za ufahamu. Pia, wanafunzi wanastahili kuhimizwa kusoma kwa mapana ili kukuza stadi za kukabiliana na maswali ya ufahamu wa kuandika.

## 4.2 SEHEMU YA PILI – INSHA

Katika mwaka wa **2014** mada ya insha ilikuwa:-

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

*Huyo alikuwa ndugu ambaye kamwe sitaweza kumsahau.*

Swali hili lilitahini uandishi wa insha bunilizi za mdokezo.. Mtahiniwa alihitajika kubuni utungo ambao unaonyesha umuhimu wa ndugu/rafiki/mhisani katika maisha yake.

**a) Maudhui/yaliyomo**

Hapa mtahiniwa alihitajika kuandika kisa ambacho kilionysha tukio/matukio ambayo yalimfanya asimsahau ndugu huyu.Yafuatayo yanaweza kuzingatiwa:

i) Ndugu yako wa kinasaba akuokoe kwenye janga/uhitaji fulani.
ii) Jirani akusaidie kuepuka hatari.
iii) Mwanafunzi mwenzako akusaidie shuleni.
iv) Afisa wa usalama akuokoe kutokana na utekaji nyara.
v) Rafiki awe nawe wakati wa furaha na wa majonzi.
vi) Mwalimu akusaidie katika kubadilisha tabia yako.



*Powered by: www.manyamfranchise.com*

**b) Muundo na mtindo**

Muundo wa hotuba ulihitajika kuzingatiwa. Yafuatayo yalitarajiwa kubainika:

**i)** **Mwanzo** – Mwanzo wa kisa ubainike.Anaweza kuanza kwa mbinu rejeshi.

**ii)** **Mwili** –Hapa ndipo mtahiniwa anapokikuza kisa chake. Matukio mbalimbali yajitokeze. Tukio moja pia linaweza kukuzwa kwa kina.

iii) Mtindo wa usimulizi ujitokeze.Uteuzi mwafaka wa tamathali za usemi na mbinu nyingine za kimtindo kama vile dayolojia za wahusika, ambazo zinalenga kukuza mada husika uzingatiwe.

iv) Kaida za kisarufi zizingatiwe.

v) Maendelezo mwafaka ya maneno yazingatiwe.

vi) Insha iandikwe kwa hati nadhifu inayosomeka.

**vii)** **Hitimisho-** Hapa ndipo msimulizi anapohitimisha hadithi yake.Atumie kauli aliyopewa kwa kuioanisha vyema na kisa chake.

**4.2.1 Vigezo vya kutathminia**

Yafuatayo ni maelezo yanayoonyesha jinsi watahiniwa wanavyotengwa katika viwango/vitengo vinne maalum, na mambo ambayo yanazingatiwa ili kumtuza mtahiniwa kiasi fulani cha alama katika vitengo hivi vinne. Vifuatavyo ndivyo vitengo (makundi) vya alama:

(i) 01 – 10
(ii) 11 – 20
(iii) 21 – 30
(iv) 31 – 40

**4.2.2 Kundi la kwanza (alama 01 – 10)**

Watahiniwa katika kitengo hiki hawamudu kujieleza katika Kiswahili. Watahiniwa wanaopata alama **01-05** hasa huwa na mtindo hafifu sana wa kujieleza. Insha zao hukosa muwala na muumano wa mawazo. Baadhi hujieleza kwa kuchanganya maneno ya Kiswahili, Kiingereza na hata lugha zao za mama. Wengine hutumia maneno yasiyoeleweka kabisa. Msamiati hutumiwa kiholela bila uwiano wowote, ama na misamiati jirani, au na mada husika. Udhaifu wao kimawasiliano huwakosesha kuikuza mada/ maudhui ya swali walilopewa.

Watahiniwa wanaotuzwa alama **06-10** hudiriki kujieleza kwa Kiswahili, japo kwa mtindo hafifu. Hata hivyo, insha zao huwa na mategu mengi ya sarufi na hijai ambayo huufifilisha usimulizi/kujieleza kwao. Hawa pia huwa wamepotoka au kupungukiwa kimaudhui/upande wa mada na wengi huhamisha sheria za lugha zao za mama hadi Kiswahili (huwa na athari nyingi za lugha ya mama).



*Powered by: www.manyamfranchise.com*

**Mtungo wa kwanza**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

Huyo alikuwa ndugu ambaye kamwe sitaweza kumsahau.

Nilikuwa na fanya kazi yangu nikiwa nimefanya duka nili sikuya kaba ndugu yangu ambaye kamwe mimi nilikuwa nime mpenda kama chaba napete kwamana yeye ni limubeba sana kasababu yeye alikuwa sikukuwa na mamena engene yakusema isipokuwa ta nilikuwa nataka kumo mandugu mimi nilikuwa nimempenda sana kama deye baba angu

Siku hiya nilisikiya kama bahi diyo sasa ameenda nilisikiya vebaya nalilisika sasa mimi nilisikiya kama ntaagoka

Sasa mimi nilikuwa nime tupa faham yangu kasababu ya vele mimi nilikuwa nafuraha tukiwa nayeye tulihisi vizuli kwa maana tulikuwa nafurah tukiwa nayeye tuki feulahay na tuki faya kazi yetu tulikuwa tukifaya kazi nilikuwa nakulika kubaoa sana kwa sababu nilikuwa nadowa mngu ata tufaya vizuli kwasababu ya kazi tulifaya kwa mikona yetu.

Sikomala ninakubuka tukiwana yeye alikuwa ame enda kufaya kazi nayeye



Powered by: www.manyamfranchise.com

alikuwa tukifanya kazi alini abiya aya kuwa akaeda [illegible] utoya kufay kazi ukamilenu kiafu asalubi tekea [illegible] kafanya kazi i ayaya teten ana tukiwa nayey tulikuwa tukifaya kazi yetu tukiwa pamaga naye alikuwa: tukifika kalibo nakwaye alikuwa ana fanya kazi tukiwa nayeye tukifu ata pahali ana elikaya nato kifaka pahali alfaya uelatoga faya kazi zuliza kila siko tuli kuwa tunaada pahali na kuketi pahali na kupu muzik hab kam hatuna mapekila mabaya.

Siku moja tulikuwa tume keti pahali chini yamuti tukiwa wawili tuli lika haponakusaha tuli kuwa ade tulika ka usa limoda kma hawogele si nani kamu liza kwanini hakuwa ana nagadese lakini niligundua kama ali kuwa malejagi akini abiya anatakaee mlgudua huya alikuwa ndogu sambaye kamwa sulaaze kumsabau,

Mtahiniwa huyu anajaribu kukisia kiini cha utungo.Ingawa ameandika kwa lugha ya Kiswahili, anayosema hayaelekei kuhusiana moja kwa moja na mada. Uakifishaji wa kazi hii ni hafifu mno. Anachanganya herufi kubwa na ndogo hata katika neno moja. Insha ina mategu mengi ya kimawasiliano ambayo yanaudhalilisha usimulizi wake.

Alama iliyotuzwa: **02**



*Powered by: www.manyamfranchise.com*

## Mtungo wa Pili

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

Huyo alikuwa ndugu ambaye kamwe sitaweza kumsahau.

Ulikuwa ni mwisho wa mwaka, ilipo tulikuwa tume funga shule. Siku moja ninangu alinambia kuwa nitaenda kwa shangazi yangu aliyekuwa anaishi mjini Mombasa. Niliposikia hivyo nilishagiria kwa furaha, kusikia kuwa nitamtembelea shangazi yangu nisilikuwa nimemwona kwa muda mrefu. Ninangu akanishawishi kuwa kesho asubuhi na mapema nitanyoa nango kuelekea mjini Mombasa.

Asubuhi na mapema siku iliyofuata nilichukuwa tauro nyangu na kuelekea hamamuni kushitaki nango, kisha nikauchukuwa mswaki na kupiga mswaki, kisha nikalejea chumbani mwangu embabo niliyangalia mavazi ya liyokuwa yakimetameta bimithiri ya yota angani, kisha nikaelekea sebureni na kumpata ninangu akiwa amekitayarisha kiamsha kingwa. Niliponaliza niliuchunguwa mgomba wangu wangu na kumwangu ninangu na kuelekea kituo cha magari. Niliposfika niliyakuta manyari yakiwa tayari ya mepiga duria ukuwa ongoja abiria waliokuwa wana safiri mjini Mombasa.



Powered by: www.manyamfranchise.com

Abiria walipofika wengeneo walikuwa wanasafiri mjini Mombasa basi liliunza safari yeme lakini dereva arikuwa yuwakiendesha kwa mwendwa kwa kasi sana sawa na umeme. safari hiyo ilikuwa refu mno ataingawa lulifika salama salimini.
Tulipofika mjini nilishanga na kupunga. sikuyamini macho yangu kwa kuona umati wa watu mjini huo.

Nilipokuwa nikitembea kwa mwendwa wa aste aste nilishtukia mgomba wangu niliokuwa nimeumbemba umenyakuliwa na kijana ambaye aliyekuwa mwizi hatari eneo hizo. nilishindwa na lakufunya wala lakutendu, huku kurikuwa kwa elekea nyakati za usiku, jaa ilinzindi hukuniikiwalu na kunazua namona abayo ngeweza kupatu chakula na mahari nigelala. usiku ulikuwa mrefu kwangu kulipokucha nilimwona kijana ambaye, aligekuwa akiyangu maji nilimkibilia na kumwomba angarao tone la maji. lakini yakushanga za nikuwa alikuwa dongu yangu wa tokani toke bila mimi kuwa na habali. damu ni zito kuliko maji alinipa yule maji, kisha akani peleka mahali ambapo nige patachakula na makazi megine mapia. kisha akani'pelека kwake.



Powered by: www.manyamfranchise.com

mkubwani niliwaimulia ambayo alikuwa
yuaishi hapa Jijini Mombasa. Huyo alikuwa
ndugu ambaye kumwe sitawasau kusahau

Mtahiniwa huyu ameielewa mada na kujaribu kuikuza kwa lugha inayoeleweka zaidi akilinganishwa na wa awali. Ingawa insha hii ni bora kuliko ya awali, mtindo wake wa kujieleza bado ni hafifu mno.

Mvuto wa insha yake umetingwa na makosa mengi ya sarufi na hijai, Mathalani:

a) **tume Funga** badala ya **tumefunga**
b) **alibokuwa** badala ya **alipokuwa**
c) **nilishangiria** badala ya **nilioshangilia**
d) **mwendwa** badala ya **mwendo**
e) **alinabia** badala ya **aliniambia**
f) **mgomba** badala ya **mkoba**
g) **dungu** badala ya **ndugu**
h) Matumizi mabaya ya kiunganishi **'ijapo'**
i) Matumizi yasiyofaa ya nyakati. Kwa mfano, **"aliniambia kuwa kesho asubuhi na mapema nitang'oa nanga...** - badala ya **'aliniambia kuwa siku ambayo ilifuata/siku ambayo ingefuata/ asubuhi ya siku hiyo ningeng'oa nanga...'**
j) **safari refu** badala ya **safari ndefu.**

Uakifishaji wake mbaya mno unaishia kuvuruga muwala wa utungo wake.

Alama iliyotuzwa: **06**

**Kundi la Pili (alama 11 – 20)**

Kundi hili huwa na watahiniwa ambao wanaimudu lugha kiasi. Wanaweza kujieleza/kusimulia kwa sentensi au kauli zinazoleta maana. Wale wanaotuzwa alama **11-15** huwa na makosa mengi ya sarufi na hijai, na insha zao hukosa mtiririko mzuri wa mawazo.Wengi huwa bado na athari za lugha za kwanza/ lugha za mama.

Wanaotuzwa alama **16-20** huwa wameimudu mada kiasi na mtindo wao wa uwasilishaji huwa bora zaidi, ingawa bado huwa chini ya wastani. Wanaweza kutumia msamiati wa kuvutia hapa na pale japo kwa kawaida wengi huutumia msamiati wenyewe vibaya. Insha zao kwa kawaida hutosheleza urefu.



*Powered by: www.manyamfranchise.com*

## Mtungo wa Tatu

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

Huyo alikuwa ndugu ambaye kamwe sitaweza kumsahau.

SIKU AMBAYO SITAWAHI SAHAU MAISHINI MWANGU

Siku hiyo niliamka saa kumi na mbili asubuhi kabla ya jogoo kuwika. Nilichukua taulo yangu na kuelekea hamamuni kwani siku hiyo tulikuwa tuna enda kutembea mji wa momba sisi mabahati wa darasa la nane. Sote tulivalia sare za shule kama tulivyo agizwa na mwalimu mkuu. Tulipo fika shuleni gari lilikuwa limefika na hapo ndipo tulipo agizwa na mwalimu mkuu bwana Ndegwa.

Bila kubananga masaa tuliingia ndani ya gari tayari kuelekea Mombasa raha. Tulipo kuwa kwenye baraste tukiendelea na safari yetu nina mmoja mkongwe alisimamisha gari yetu na kumueleza dereva kama anaweza kumsaidia kwakuwa yeye asiki vizuri. Kwa huruma mwalimu mkuu alimuagiza aingie ndani lakini sisi tuna fika mombasa.

"Ta! ta! ta!" sauti ya bunduki ilisikika nyuma sote tulishikwa na butwaa kusikia sauti hiyo basi dereva kaamua kuendesha gari kwa mwendo wa kasi lakini hiyo haikukuwa mwisho wa visa mle mle tu tukali gari lingini ne mbele yetu ilikuwa ni trela tuliogopa sana kwani ilikuwa siku ya kwanza kuondokewa na kisa hicho tokiwa tuna safiri. Ndereva aliamua kupiga kona kwa kuwa yeye



Powered by: www.manyamfranchise.com

pia alishikwa na butwa kuona hilo gari lingine. Nderева alipokuwa akipiga kona yule nina aliye kuwa ndani ya gari lelo alitoa binduki na kuagiza kila mtu apige magoti chini.

Lo! kumbe yule hakuwa ni mwanamke bali alikuwa ni gulamu alikuwa anakaa kanakwamba ako na miaka kumi na saba ni vile tu alikuwa anashirikiana na genge la wezi. Lile gari lililo kuwa nyuma yetu ilikuwa imewabeba wezi walioondoka wote nje na kutueleza tuinuwe mikono juu. Tuliyainua mikono yetu juu huku roho yangu ikidunda dududu. Walitupeleka kati jumba jingine lililo kuwa kando ya barabara tulielekea humo sisi sote tukiwa tumeandamana kama siafu.

Kwa kweli wahenga na wahenguzi hawakutuchana kwa mfupa wasemaki walipoDena siku ya mwizi ni arubaini. Iliwadia siku hiyo ambapo ghulamu mmoja alikuwa akielekea shambani pake alipokuwa akienda aliwapata wale wezi kando ya barabara akawasikia wakisemezana wakisema yakwamba siku imewadia ambapo tunafaa kuchoma wale wanafunzi tulio wateka nyara kwa kweli yule mvulana alikuwa mzuri sana aliniona pale kwa dirisha na kuniuliza nini ni na fanya pale nika mueleza nimetekwa nyara nikamuomba usaidizi kwa kweli alinisaidia alitufungulia mlango na



Powered by: www.manyamfranchise.com

enda hadi kwa polisi na hapo ndipo tulipopata usaidizi na kweli huyo alikuwa ndugu ambaye kamwe sitaweza kumsahau.

Mtahiniwa huyu anaonyesha kuielewa mada zaidi ya wale wa awali. .Hata hivyo, utungo wake umejaa makosa ya sarufi na hijai ambayo yanaufanya kuwa hafifu. Makosa ya kihijai, kimsamiati , kimuundo na kisarufi yanayojitokeza ni kama vile:

a) **tunaenda** badala ya **tunaenda**
b) **ndereva** badala ya **dereva**
c) **anaweza** badala ya **angeweza**
d) **aingie ndani lakini sisi tunafika Mombasa** badala ya **aingie, japo tulikuwa twaelekea Mombasa**
e) **nina** badala ya **mwanamke**
f) **hiyo haikuwa mwisho,** badala ya **huo haukuwa mwisho**
g) **Tuliyainua mikono yetu** badala ya **tuliiinua mikono yetu**
h) **haikukuwa** badala ya **haikuwa**

Uakifishaji wake ni mbovu.

Alama iliyotuzwa: **12**

**Mtungo wa Nne**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

Huyo alikuwa ndugu ambaye kamwe sitaweza kumsahau.

Mimi ni mtoto wa pili wa nina yangu. Nina ndugu wawili. Kifunguamimba kwa jina ni Muemi na kifunga mimba ni Jaki. Sisi tulipendana kila wakati utotoni. Tulishirikiana kama jembe na mpini kwa kila kazi tuliyopewa nyumbani na mama yangu. Kila tulipotumwa dukani, tulifuatana unyounyo mithili ya mfu waendao kuhemela.

Muemi alikuwa amemaliza kidato cha nne kwani, aligonjea kuelekea chuo kikuu. Mwaka uliisha na akaelekea chuo kikuu ambako akaendelea na masomo yake. Masomi,



Powered by: www.manyamfranchise.com

alitia bidii kama za mchwa ajengaye kichunguu. Hakuchoka na ndipo akamaliza masomo yake na baadaye aliajiriwa. Kila mwezi alizipata pesa chungu nzima.

Pesa alizopata alinielimishia pamoja na ndugu yangu Joki. Aliwajengea wazazi wangu jumba kubwa na kuwapa kila walichohitaji. Kila asubuhi mama yangu alitiririkwa na machozi ya furaha kwa kuwa vyote alikuwa navyo. Naye baba aliabiri matwana ya furaha kama bunda yaliyerauka na kudamka na kupata magego

na shingo lake lilikosa mifupa na kusunguka kila upande, kwa utesi si kidogo. Alikumbuka vile alivyomuelimisha Mueni kwa dhiki; kwa wakati mwingi jenje zilikuwa neno lililotiwa kamusini kimakosa.

Baada ya miaka miwili, Mueni aliugua na akalazwa hospitalini. Magonjwa yalimfamia kama vile nzige walifamia lo shamba la mihogo. Alijaribu kutibiwa lakini matumaini hayakuonekana.

Ilikuwa asubuhi saa tatu tulipopata habari kuwa ndugu yetu amesafiri jongomeo bila matwana wala nauli. Walezi wangu walilia kwa uchungu mwingi hadi nina akasirahi. Hapo ndipo



Powered by: www.manyamfranchise.com

nilijua kuwa walendi wa lugha hawakutupako mafuta kwenye tako la chupa walipanena, ukistaajabu ya Musa utayaona ya firauni. Nilihisi uchungu mwingi huku machozi yakinitililika bwaibwai na kugwaya kama ndege mgo kwao.

Nilijua kuwa nina yangu naye ataifuata njia ile. Woga ulinitawala pakubwa. Baada ya kugedere kuchupa kwenye utaga wa mkonju hadi kwenye ukaju wa msonabari, nina yangu alipata fahamu na kuamka.

Maisha yangu sasa yalikuwa katika hatari kwani singeendelea na masomo tena. Pesa zilikosa.

Mungu hamsahau mja wake. Msamalia mwema alijitolea na kunifunza. Nilipoona hayo nilimshukuru rabishtani wa rehema kwa kuwa nilipata wa kunifunza. Nami nilitia bidii na nikahitimu masomo yangu. Sasa mimi ni mkurugenzi mkuu wa benki kuu ya Kenya. Mimi huwasaidia watoto ambao walezi wao hawana uwezo wa kuwasomesha.

Mimi kwamwe humuhitaji ndugu yangu kwani alinisaidia sana kimaisha hata kama alisafiri jongomeo. Huyo alikuwa ndugu ambaye kamwe sitaweza kumsahau.



Powered by: www.manyamfranchise.com

Mtahiniwa huyu amebainisha kuimarika zaidi.Anaitumia lugha kwa wepesi zaidi akilinganishwa na wa awali. Ameielewa mada na kuiwasilisha kwa mtindo wa kiwango wastani. Hata hivyo, hajaikuza mada ipasavyo.Makosa ya kisarufi na hijai ni kama vile:

a) **aligonjea** badala ya **alingojea**
b) **alitililikwa** badala ya **alitiririkwa**
c) **kichunguu** badala ya **kichuguu**
d) **ambako akaendelea** badala ya **ambako aliendelea**
e) **kifungua mimba kwa jina ni** badala ya **kifungua mimba anaitwa**
f) **shingo lake** badala ya **shingo yake**
g) **yalimfamia** badala ya **yalimvamia**
h) **kwamwe** badala ya **kamwe**

Insha ina makosa mengi ya kimuundo. Pia mtahiniwa huyu anapachika msamiati

Alama iliyotuzwa: **18**

**Kundi la Tatu (Alama 21 – 30)**

Insha katika kitengo hiki huwa inaeleweka vizuri. Hudhihirisha kiasi fulani cha ukomavu wa mawazo. Huwa na mshikamano na mtiririko mzuri kiasi wa mawazo. Insha zinazotuzwa alama **21-25** huwa na ubunifu wa kima cha wastani.Aghalabu watahiniwa hupoteza alama kupitia makosa ya sarufi na hijai, matumizi mabaya ya tamathali za usemi na uakifishaji mbaya. Hata hivyo,, mtahiniwa huwa ameikuza mada vizuri.

Insha zinazotuzwa alama **26-30** huwa na ukomavu zaidi wa mawazo. Maudhui hushughulikiwa kikamilifu zaidi na huwasilishwa kwa mtindo unaovutia zaidi. Insha katika kijitengo hiki hutosheleza urefu.Hata hivyo, insha hizi bado huwa na makosa kiasi ya sarufi na hijai.



*Powered by: www.manyamfranchise.com*

Mtungo wa Tano

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

**Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.**

**Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:**

**Huyo alikuwa ndugu ambaye kamwe sitaweza kumsahau.**

Ilikuwa siku ya Jumamosi nyakati za likizo. Mama mzazi alinituma dukani kwenda kununua bidhaa za sherehe ya siku iliyofuata. Niliendа shoti ili nipate mwenye duka kabla hajafunga.

Katika zile harakati zangu za mbio niligonga bhaibu mmoja aliyekuwa akinisubiri kwa mawazo yangu. Alikuwa gofu la mtu na mrefu kama mlingoti, mwenye macho kama ya gololi.

Alinitazama kwa hasira nyingi sana. Niliomba msamaha na kisha kwenda zangu. Punde si punde gari la wanapolisi likija na kunitumbukiza ndani kwa haraka.

Haraka haraka haina baraka. Gari lenyewe lilitiwa moto na kuwacha vumbi likirea juu angani. Nilipoangalia nyuma nilimwona ghulamu mmoja kwa baiskeli huku akitufuata.

Baada ya safari hiyo tulitia nanga tulikokuwa tukielekea. Nilitolewa kama gunia la viazi. Nilijaribu kusema nilichotoka lakini hakuna aliyeshughulika.

Sikuweza kupiga kamsa kwani kinywa



*Powered by: www.manyamfranchise.com*

changu kilikuwa kimefungwa na kitambaa chenye harufu iliyonidhuru mapua. Kuingia kule ndani, sakafu lenyewe lilikuwa bandi kama barafu, lenye kung'ara kama dhahabu.

Sikufahamu kilichokuwa kikitendeka. Muda usio na kifani ghulamu yule yule akajitoma ndani kwa hasira huku jasho likimtiririka tiriri.

Nyuma ya mfuko wake alibeba bunduki na risasi zisizojulikana kwa rangi. Wale majambazi walimwangalia kwa masikitiko na huruma.

Lakini yeye kilichomleta hapa hakikujulikana kamwe. Punde si punde wote walikuwa sakafuni mahututi huku damu ikiwatiririka tiriri kama maji.

Nilihofia sana yule ghulamu. Sikujua nia yake ya kutenda haya wala majambazi. Aliponikaribia nilisonga na matako huku nikitetemeka kila sehemu.

Alinieleza nia yake ya kuja hapa na kuwapa tunzo wale majambazi. Aliponikaribia, kabla ya yeye kunifungua jambazi mmoja alirukia bunduki, iliyokuwa nyuma ya mfuko na kumfyatua risasi.

Nilimwangalia akiaga dunia. Huyo alikuwa ndugu ambaye kamwe sitaweza kumsahau.



Powered by: www.manyamfranchise.com

Mtahiniwa huyu amedhihirisha kuwa ameilewa mada na kuiwasilisha kwa mtindo bora zaidi akilinganishwa na wa awali. Huyu pia ana makosa mengi ya sarufi, hijai, kimuundo na kimsamiati. Kwa mfano:

a) niligonga shaibu aliyekuwa akinisubiri kwa mawazo yangu
b) matumizi mabaya ya **na,** kwa mfano **na kitambaa,** badala ya **kwa kitambaa**
c) msamiati usiofaa, kwa mfano, **wanapolisi** badala ya **polisi**
d) **likijaa** badala ya **likija**
e) Kushopeka msamiati, kwa mfano **haraka haraka haina baraka**
**f)** **safu lenyewe** badala ya **sakafu yenyewe**
**g)** **aliubeba bunduki** badala ya **aliibeba bunduki**
**h)** **nilihofya jana** badala ya **niliihofia nia**

Aidha, uakifishaji usiofaa, kutohusiana kwa mawazo kimantiki, kuchopeka msamiati, na ukosefu wa muwala, unaivuta nyuma kasi ya uwasilishaji na kuipoka insha mvuto.

Alama iliyotuzwa: **21**



*Powered by: www.manyamfranchise.com*

Mtungo wa Sita

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

**Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.**

**Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:**

**Huyo alikuwa ndugu ambaye kamwe sitaweza kumsahau.**

Kwa miaka kadhaa kijiji chetu hakikuona tone la mvua kutoka angani kutua ardhini. Labda waja walikuwa wamemwasi Mterehemezi na kwa hivyo alikuwa anawaadhibu kwa ukame. Mifugo walifariki kwa ukosefu wa lishe huku mimea ikinyauka.

Hata hivyo nawaruhia kofia wahenga waliposema msemo usemao hakuna marefu yasiyo kuwa na mwisho. Kipindo hicho kirefu cha kiangazi kilifika tamati kaski moja! Tulikuwa skuli darasani pale mawingu mepesi yalipojikusanya na kuunda wingu kuu jeusi angani lililokiacha kijiji cha kijito nyama kwenye giza totoro.

Mvua si kidinya wingu hilo lilipasuka na kuangusha tone baada ya tone na hatimaye mvua yenyewe ikaanza kunyesha. Ilinyesha kwa matone mazito mazito kwa muda wa saa



Powered by: www.manyamfranchise.com

One hivi. Ilipoacha kunyesha mabwawa yalikuwa yamejaa kila mahali. Hali hii ilimlazimu Mwalimu Mkuu kutuachilia twende manzilini mapema kuliko kawaida. Bila kupoteza wakati, tuliipachika mikoba yetu kwapani kushika njia.

Njiani tulikutana na yaliyotuacha vinywa wazi. Kijito tulichokuwa tukivuka kila siku kilikuwa kimefurika na kuwa jito. Maji yaliyojaa pomoni yalilisomba daraja letu la pekee. Tulibaki bila namna ya kuvuka. Maswali yalikuwa yakitulewalewa kichwani tusijue la kufanya.

Baada ya kuwaza na kuwazua, wazo lilinigonga kichwani. Wazo hili lilipingwa na kila mtu. Kakangu mkubwa aliniona nisithubutu kuhatarisha aushi yangu lakini hayo hayakunipiga mshipa. Nitia masikio nta na kukata shauri kupiga mbizi na kuuvuka mto huo. Waambao husema mwenye nguvu mpishe. Niliwasahau wasemao usemao kuwa



Powered by: www.manyamfranchise.com

asiyesikia la mkuu huvunjika
guu.
Nilijitosa mtoni kama
hodari na kutumbukia. Wenzangu
walitarajia kuniona lakini bure
halikutokea. Dakika chache waliniona
juu ya maji nikipelekwa kwa
mwendo wa kasi. Nilitapatapa
lau nife maji lakini nilimkulia
bahati. Kakangu aliruka kuja
kuniokoa na juhudi zake zikazaa
matunda. Ningependa [illegible]
Pesi [illegible] wala [illegible].
[illegible] Ama kweli, [illegible] kweli
alinijalia. Huyu alikuwa ndugu
ambaye kamwe sitaweza kumsahau
hau.

Mtahiniwa huyu amebainisha ukomavu zaidi akilinganishwa na wa awali.Ameielewa mada na kuiwasilisha kwa mtindo mzuri wenye mvuto kiasi. Amebainisha wepesi wa kuitumia lugha kukikuza kisa chake.Anatumia msamiati mwafaka kama vile walifariki, lishe, nawavulia kofia. Hata hivyo, insha hii bado ina makosa ya kihijai, kisarufi na msamiati.

Kwa mfano,

a) **maan zili-ni** badala ya **maanzilini**
b) **yali lisomba** badala ya **yalilisomba**
c) **yameja** badala ya **yamejaa**

Aidha, kuna matumizi mabaya ya msamiati, kwa mfano, **kupachika mkoba kwapani** badala ya **kupachika mkoba begani.** Kadhalika, badala ya kulenga mada moja kwa moja, anaanza kusimulia kuhusu kutonyesha, jambo ambalo linavuta kasi ya usimulizi na kuipweza thamani ya kazi kiumbuji yake.

Alama iliyotuzwa: **25**



*Powered by: www.manyamfranchise.com*

**Kundi la Nne (Alama 31 – 40)**

Watahiniwa katika kundi hili kwa kawaida huwa wanaimudu lugha vizuri. Huwa na kiwango cha juu cha ubunifu kimaudhui na kifani. Hutumia lugha kwa wepesi kujieleza. Mijadala au masimulizi yao huwa na muundo bayana wenye mshikamano na mtiririko mzuri wa mawazo. Hawa huielewa mada na kuikuza kwa kiasi cha kuridhisha. Wale wanaotuzwa alama **31-35** huitumia lugha kwa wepes zaidi. Hata hivyo, insha zao huwa na makosa ya hapa na pale ya sarufi, hijai na msamiati.

Wale wanaotuzwa alama **36-40** huwa na umilisi wa lugha wa kiwango cha juu zaidi na huwasilisha mawazo yao kwa mitindo mbalimbali ya usimulizi au mitindo mbalimbali ya kujieleza ambayo huzipa kazi zao mvuto wa hali ya juu. Huteua msamiati unaoafiki mada na kuutumia vyema kufanikisha usimulizi au mjadala wao. Insha zao huwa na makosa machache mno ya sarufi, hijai na msamiati. Hali kadhalika hati zao zinasomeka kwa urahisi na wanatosheleza urefu.

**Mtungo wa Saba**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

AKUFAAYE KWA DHIKI NDIYE RAFIKI.

Huyo alikuwa ndugu ambaye kamwe sitaweza kumsahau.

Shangwe na nderemo zilihinikiza hewani. Yote hayo yalidhihirisha upeo wa furaha na bashasha ya akina mama. Siku iliyosubiriwa kwa hamu na dukuduku kuu hatimaye iliwadia. Harufu nzuri ya michuzi rojorojo iliyoandaliwa kwa sherehe, ilinukia. Nilifahamu fika kwamba mambo yote yalikuwa yamepangwa yakapangika.

Bila kupoteza wasaa, nilizitoa magwanda niliyokuwa nimevaa na kuvalia kitenge changu cha rangi ya hudhurungi yenye maua ya waridi. Machozi yalinilengalenga machoni pangu kwa sikitiko na wasiwasi wa mwasi. Kwa nini haya yanitendekee? Maisha yangu ya masomo yalifikia hatima ya ghafla, wavyele wangu walipoamua kunioza kwa zee lililobugia chumvi si haba.



Powered by: www.manyamfranchise.com

Nilikuwa banati wa miaka kumi na miwili mwenye tumaini la kukamilisha masomo. Maazimio yangu yote yalikuwa yamegonga mwamba. Ilibidi nifunge akidi na zee hilo kwani lisilo budi hubidi.

Vigelegele na mbwembwe hazikukauka nilipotoka katika chumba changu. Wanawake walijipamba kwa chale na ndonya. Nilipoangalia angalia, niliwaona masahibu zangu. Nilimwona mwandani wangu wa dhati, Msaada Urafiki wangu na sahibu yangu ulikuwa wenye utanisi. Aliniauni kwa moyo wake karimu. Hakuwa na kinyongo kama wengine. Alikuwa kama ndugu yangu kwani tulikuwa na urafiki wa kula na kusaziana. Alinitupia jicho la huruma nisijue la kufanya. Hiyo ilikuwa ishara kamili kwamba hakuwa na mbinu ya kuninusuru.

Mbele kidogo, palisheheni wazee ambao labda, walijadiliana kuhusu mahari. Nilihisi kuwasihi wasinioze lakini hii ilikuwa mwiko. Nilisalia pale nimejinyamazia ji huku nikijijazia maneno. Bwana Mzee aliyekuwa anioe aliwasili. Alivalia suti nyeusi pengine kuashiria ubaya wa siku hiyo. Ama kwa kweli nyeusi ni jazanda ya uovu na bila shaka huo ulikuwa uovu usiokadirika.



Powered by: www.manyamfranchise.com

Bwana Mzee alijikokota kwa mkongojo aliokuwa nao mkononi. Marafiki zangu, isipokuwa Msaada, walicheka kwa dharau na beza. Jambo hilo lilinitia hamaki na kero. Kama ilivyokuwa desturi za hapo kijijini, mkuu wa masuala ya kidini aliuliza iwapo kulikuwa na pingamizi lolote. Kimya kikatomalaki kisha kwa ujasiri mkubwa, Msaada akasimama.

"Ninapinga harusi kuendelea. Mimi ni mwanafunzi na baada ya kufunzwa, nimeelewa kwamba, hii ni mojawapo ya tamaduni zilizopitwa na wakati. Kwa nini mmwoze gashi mwenye umri mdogo kama huyu? Kwa nini mmharibie mustakabali wake? Tafadhali, tuelimike na tuache kufuata mila hizi. Hata kama mwacha mila ni mtumwa, haifai kuwaharibia wasichana maisha yao ya usoni. Tumakinike na tusiwaoze wana wetu kamwe. Ninawasihi msimwoze rafiki yangu, Sikitiko," alisema kwa ujasiri.

Pindi alipomaliza, niliachwa nikiduwaa. Nyuso za waliopanga harusi hiyo zilijiinamia shabiku ya lililonyauka kwa tahayuri. Hii ilikuwa ishara tosha kuwa nisingeozwa. Furaha ilinitinga moyoni. Nilimshukuru na kumpiga pambaja rafiki yangu. Nilimshukuru Rabuka kwa kumleta Msaada sherehe ni pale. Huyo alikuwa ndugu ambaye kamwe sitaweza kumsahau.



*Powered by: www.manyamfranchise.com*

Mtahiniwa huyu ameilewa mada na kuikuza kwa lugha komavu zaidi akilinganishwa na wa awali. Anajieleza kwa wepesi zaidi akilinganishwa na wale wa vitengo vya chini. Ameteua msamiati mwafaka kulingana na mada yake.Mifano ya msamiati huu ni: **maazimio, hatima, yamegonga mwamba, nifunge akidi, jazanda, bezo.**

Aidha ametumia mbinu nyingine za kimtindo kama vile maswali ya balagha , majazi, na taashira.

Insha hii ina makosa machache ya sarufi, hijai na uakifishaji. Baadhi ni:

a) **nilizitoa magwanda** badala ya **niliyatoa magwanda**
b) **hii ni mojawapo ya tamaduni** badala ya **huu ni mmojawapo wa tamaduni**

Alama iliyotuzwa: **32**

**Mtungo wa Nane**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

NDUGU NI KUFAANA SI KUFANANA

Huyo alikuwa ~~ndugu ambaye kamwe sitaweza kumsahau.~~

Machozi yalinipukutika puku puku kama mgomba. Sikuyaamini wala kuyasidiki macho yangu nilipomwona kako yangu akiwa amelalishwa katika mochari, akiwa mwendazake. Niliyawa na huzuni mpwito mpwito. kaiti ningalimthamini kama alivyotakikana. kaiti ningalisikia maneno yake ya busara. Chambilecho wahenga, majutu ni mjukuu.

Fikira zangu zilirudi nyuma. Nilikumbuka maisha yangu ya kisogoni na vile kaka yangu alinifaa kwa hali na mali. Nilipokuwa mtoto mchanga, dau la maisha la wazazi wangu lilitia nanga. Mimi na kaka yangu tukakuwa mayatima. Hatukuwa na mbele wala nyuma. Tulikabiliana na matatizo chungu nzima. Waama, aliyeachwa, kaachiwa mengi.



Powered by: www.manyamfranchise.com

Kaka yangu akaajiriwa kazi ya uhamali ili aweze kunipa mahitaji mbalimbali. Alifanya kazi kwa bidii za msumeno kukereza mbao licha ya mshahara duni. Uzembe na uzohali alivitupa katika kaburi la sahau. Daima hakuwa kupe kutia mrija kwa wengine. Aliamini fika kwamba mchumia juani hulia kivulini.

Wakati niliugua, alifanya lolote na chochote ili kuhakikisha nilipata matibabu. Mara nyingi alilalia mate ili nipate angalau chakula kidogo. Alinipenda kama mboni za jicho. Alipoona nikikanyaga chechele, hakusitasita kunishika sikio kwani ukichelea mwana kulia, utalia mwenyewe.

Wahenga hawakukosea walipoena kwamba asante ya punda ni mateke. Nilipokua, nilijawa na utundu na kuwa mkaidi kama mkia wa nguruwe. Nilizitemea mate nasaha za kaka yangu. Alipojaribu kunirudi, nilimtolea maneno yaliyopenya moyoni kama mshale wa sumu. "Kwa nini aniadhibu na yeye si mzazi wangu?" nilijiuliza kila mara.

Licha ya ujeuri wangu kaka yangu alizidi kunipa wosia. Nilitia pamba masikioni na kujiunga na walanguzi wa dawa za kulevya. Tabia yangu ikazidi kudorora



Powered by: www.manyamfranchise.com

huku uovu ukistawi. Kaka yangu akakuwa binadamu asiyekuwa na maana kwangu. Alinipenda na kujaribu kadri ya uwezo wake kunishika sikio lakini wapi? Sikio la kufa halisikii dawa.

Siku moja nilipokuwa katika nyumba ya mlaguzi mkuu wa dawa za kulevya, mambo yalienda shoro bin shoto.

Mfyatuko ya risasi ilisikika nje ya nyumba yake. Moyo ulinidunda du du du kiasi cha jirani kusikia. Nilitoka shoti mithili ya mja aliyefukuzwa na dinosa. Polisi waliokuwa nje wakaanza kutufuata kwa kasi.

Kaka yangu aliyekuwa akifanya kazi yake ya uhamali aliniona nikikimbizwa na polisi. Aliwacha mkokoteni wake na kunifuata mbio mbio ili ajaribu kunisalimisha roho. Kwa ndege mbaya, nilijikwaa na kuanguka chini pu! Nilifumba macho tayari kuangamizwa jongomeo. Risasi ilifyatuliwa lakini sikuhisi uchungu.

Nilifumbua macho na kumkuta kaka yangu amelala sakafuni, risasi ikiwa imepenya moyoni. Kwa muda wa kubana na kubanua, alirudisha kope kwa mwenyewe. Nililia kilio cha mbwa



Powered by: www.manyamfranchise.com

mdomo juu. Niliia kama mfiwa. Kaka yangu alikuwa amepokonywa maisha yake ili kuninusuru. Kweli damu ni nzito kuliko maji.

Niligutushwa kutoka fikira zangu na polisi waliokuja kunipeleka rumande. Kweli huyo alikuwa ndugu ambaye kamwe sitaweza kumsahau.

Mtahiniwa huyu ameielewa mada na kuikuza vyema na kwa ukomavu zaidi kimaudhui na kifani. Tofauti na watangulizi wake.Uteuzi wake wa mtindo unaipa insha yake shani ikilinganishwa na za awali.Anatumia vipengele vya kimtindo kama vile mbinu rejeshi na ulinganishaji kwa ufanifu bila kuvuruga muwala na muumano wa mawazo yake. Tofauti na watangulizi wake, anahisika zaidi kuwa anawasiliana na hadhira yake moja kwa moja Mawazo yanatiririshwa kimantiki bila kukatizwa kwa uchopekaji mwingi wa msamiati ambao ulibainika katika insha za vitengo vya chini. Makosa ya kisarufi ni kama vile, **amelalishwa** badala ya **amelazwa, mlaguzi** badala ya **mlanguzi, ni kikimbizwa** badala ya **nikikimbizwa, kuangamizwa jongomeo** badala ya **kuangamiziwa jongomeo.**

Kwa jumla hii ni insha ambayo ina uasilia na inaweza kuaminika kuwa ubunifu asilia wa mtahiniwa wa kiwango hiki.

Alama iliyotuzwa: **34**

## 4.3 MAPENDEKEZO KWA WALIMU

4.3.1 Walimu wawahimize wanafunzi kufanya mazoezi zaidi katika mada tata za sarufi.

4.3.2 Ufunzaji wa msamiati uhusishwe na muktadha badala ya kuufunza ukiwa mkavu. Kwa mfano, msamiati wa magonjwa unaweza kufunzwa kwa kutumia ufahamu kuhusu magonjwa.Hili litamwezesha mwanafunzi kuuelewa msamiati katika matumizi halisi.

4.3.3 Wanafunzi wahimizwe kutumia ujuzi wa waliyosoma katika ufahamu kujibu maswali ya ufahamu badala ya kukariri au kuchopoa mawazo moja kwa moja kutoka kwenye vifungu.

4.3.4 Wanafunzi wahimizwe kutumia mbinu bora za kuukabili ufahamu. Badala ya kusoma swali, kisha kuanza kutafuta majibu, wasome ufahamu kwanza kabla ya kuyasoma maswali na majibu yaliyotolewa.

4.3.5 Walimu watunge maswali yanayopima stadi mbalimbali (ngazi/viwango) tofautitofauti za maarifa au utambuzi wala si stadi ya kukariri/ujuzi pekee. Hili litamzoesha mwanafunzi kujibu maswali ya aina tofautitofauti katika mtihani.

4.3.6 Stadi ya kusikiliza na kuzungumza ihimizwe zaidi kupitia utambaji, mijadala na imla, ili kuboresha maendelezo na kuimarisha mitindo ya kujieleza au mitindo ya usimulizi..



Powered by: www.manyamfranchise.com

4.3.7 Wanafunzi wasisitiziwe umuhimu wa kusoma vitabu na makala mbalimbali ili kukuza ubunifu.

4.3.8 Wanafunzi waonywe dhidi ya kushinikiza msamiati usiohitajika katika insha. Hili hufifilisha mawasiliano na kuifisidi insha mvuto wake.Msamiati unaoteuliwa sharti uoane na mada na kuafikiana na msamiati au matini jirani katika sentensi ambamo umetumiwa.Msamiati wa kishairi usitumiwe kuandika tungo zisizo za kishairi.

4.3.9 Walimu warejelee vitabu mbalimbali vilivyopendekezwa, wasitumie kimoja tu.Hili litawapa wanafunzi uwanja mpana wa kujifunzia.

4.3.10 Walimu wawasisitizie wanafunzi umuhimu wa hati nzuri ili kurahisisha usomaji na usahihishaji wa insha zao na kuzipa kazi zao mvuto chanya.

4.3.11 Walimu wawahimize wanafunzi kutumia Kiswahili zaidi katika mazungumzo yao ili kuimarisha mikakati ya kujieleza na kusimulia kwa kwacho.

4.3.12 Walimu wawaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufasiri mada/maswali mbalimbali ili kukinga dhidi ya kupotoka kimaudhui.

4.3.13 Walimu wawape wanafunzi mazoezi ya mitindo tofautitofauti ya insha ili wapate uzoefu wa kuandika aina mbalimbali za insha.

4.3.14 Walimu watumie mwelekeo mseto katika ufunzaji wa mada mbalimbali, kwa mfano mada changamano za kisarufi. Mathalan, mwalimu anaweza kutumia vitabu vya hadithi kufunzia dhana za kisarufi kama vile njeo, hali na aina za maneno. Hili litakinga dhidi ya wanafunzi kuziona dhana hizi kuwa dhahania. Itakuwa rahisi kuzielewa dhana hizi zikitokea katika matumizi halisi. Kadhalika hili litayafanya mafunzo ya sarufi kuwa ya kuvutia zaidi, hivyo wanafunzi watayachangamkia na kuyaelewa zaidi.



*Powered by: www.manyamfranchise.com*